THE NELSON MANDELA
AFRICAN INSTITUTION OF SCIENCE AND TECHNOLOGY
(NM-AIST)

CHAIRMAN OF THE COUNCIL'S SPEECH FOR THE 6th GRADUATION CEREMONY AT THE NELSON MANDELA AFRICAN INSTITUTION OF SCIENCE AND TECHNOLOGY

29th August 2020

HOTUBA YA MWENYEKITI WA BARAZA LA TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA YA NELSON MANDELA, MHESHIMIWA PROF. JOSEPH RWEGASIRA BUCHWEISHAIJA KATIKA MAHAFALI YA SITA, KAMPASI YA TENGERU, ARUSHA, SIKU YA JUMAMOSI, TAREHE 29 AGOSTI 2020.

- Mkuu wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela na Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal;
- Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mhe. Idd Hassan Kimanta;
- Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mhe. Jerry Muro;
- Wajumbe wa Baraza la Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela;
- Viongozi wa Kiserikali na Viongozi wa Kidini;
- Makamu Wakuu wa Vyuo na wawakilishi wa Vyuo mbalimbali na Taasisi za utafiti waliopo hapa;
- Wafanyakazi na wanafunzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST);
- Wahitimu;
- Waandishi wa Habari;
- Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,

Kwa niaba ya Baraza, uongozi, wafanyakazi, wanafunzi na jumuiya nzima ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela, napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha wote katika sherehe za mahafali ya Sita katika Chuo hiki. Niwashukuru wote kwa kutenga muda wenu ili

kufanikisha tukio hili pamoja na majukumu mengi mliyokuwa nayo.

Napenda pia kuchukua nafasi hii kuwakaribisha katika sherehe hii wageni wote waalikwa, wazazi, marafiki na majirani wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. Baraza la Taasisi hii linawashukuru kwa ushirikiano mnaoendelea kuuonyesha kwa njia mbalimbali. Kutokana na hilo ninaguswa kuwakaribisheni wote wakati huu muhimu kwa maisha ya wahitimu, wazazi, marafiki na Jumuiya ya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) kwa ujumla.

Mahafali ni tukio ya kuheshimika katika maisha haswa kwa wale waliofikia elimu ya juu katika Vyuo na Taasisi. Kwa Taasisi yetu, hii ni siku maalum na muafaka inayotengwa kutunuku shahada za uzamili na uzamivu kwa wanafunzi wanaostahili. Ni sherehe ambayo wanafunzi wanatambulika kwa vipaji na uadilifu katika fani mbalimbali. Tukio hili limefanikiwa kutokana na jitihada pamoja na kujituma kwa uongozi wa Chuo, wanataaluma na wafanyakazi kwa ujumla. Tunatambua, tunathamini na kushukuru michango yenu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo;

Ni mwaka jana tu, mwezi wa nne tulikukaribisha kwa tukio kama hili katika mahafali ya tano. Hivyo basi, leo hii ninayo furaha kukutambulisha kwako wahitimu wapatao **121;** kati ya hao, **86** ni wa shahada ya **Uzamili** na **35** ni wa shahada ya **Uzamivu**. Wahitimu wanaohitimu leo, wengi wao walisajiliwa mwaka wa masomo 2016/2017 kwa Shahada ya Uzamivu na mwaka wa masomo 2017/2018 kwa Shahada ya Uzamili. Tunajivunia mafanikio haya makubwa na ya kihistoria. Wahitimu hawa ni

mashahidi kuwa Taasisi hii imewaandaa vyema kitaaluma na hivyo wamepata ujuzi wa kutosha. Baraza linaamini kuwa wahitimu hawa wameandaliwa vyema kitaaluma kuweza kutatua changamoto za kijamii na za viwanda. Ni imani yetu kuwa watakuwa ni chachu ya mabadiliko chanya katika jamii. Ninayo furaha kuwapongeza wahitimu hawa kwa kupambana bila kuchoka hadi kufikia siku ya leo. Haikuwa kazi rahisi kwao kuwa kama walivyo leo. Mtaalamu mmoja wa masuala ya falsafa aitwae *Mike Finley*, aliwahi kusema, na nitamnukuu kwa lugha ya kiingereza ili nisibadilishe maana halisi "***Find ways around the obstacles in your life. The power lies within you and your ability to change the way you think and act. Never forget that, and never give up***." Nawapongeza sana kwa kupigana vita hivi hadi kufanikiwa kutunikiwa leo shahada zenu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo;

Kwa upande wa uwezo wa rasilimali watu katika Taasisi, idadi ya wanataaluma imekuwa ikiongezeka ndani na hata wale ambao wanatoka nje ya Taasisi kufundisha kwa muda mfupi (part time teaching). Ili Taasisi iweze kufaidika na utaalamu na ujuzi mbalimbali kutoka Taasisi mbalimbali, Taasisi ya Nelson Mandela (NM-AIST) inafanya ushirikiano na Taasisi mahiri na maarufu toka nchi mbalimbali duniani zikiwemo; USA, Canada, China, Korea na India. Pia Taasisi imejenga ushirikiano na Taasisi za ndani zikiwemo; Chuo cha Sokoine cha Kilimo, Southern African Centre for Infectious Disease Surveillance, Ifakara Health Institute, Mikocheni Agricultural Research Institute, Biosciences Eastern na Central Africa-International Livestock Research Institute, and Central African Council for Scientific and Industrial Research.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo;

Malengo ya baraza ya kuitangaza Taasisi yamejikita katika kutoa mchango wa kipekee katika kutatua changamoto za kisayansi, kiuhandisi na teknolojia zinazo ikabili jamii na viwanda. Hivyo, Taasisi imefanikiwa katika kutekeleza kauli mbiu ya *"Academia for Society and Industry",* au kwa lugha ya Kiswahili "*Taaluma kwa jamii na viwanda*". Kama Taasisi ambayo imejikita katika utafiti na ubunifu, imeweza kuchipua watafiti na wabunifu wenye kumudu ushindani katika viwango vya kimataifa na kutengeneza bidhaa mbalimbali pamoja na kutoa suluhisho katika kilimo, viwanda na biashara, kutoa mapendekezo ya kisera na kiutendaji. Matokeo ya kazi hizi yatawawezesha wahitimu kujipatia vipato na maendeleo endelevu kwao binafsi na kwa taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo;

Kwa kuzingatia kauli mbiu yetu, "*Taaluma kwa jamii na viwanda*", Taasisi imeunda ushirikiano baina ya Taasisi na wadau mbalimbali "*Nelson Mandela Public Private Partnership (NM-PPP*)" kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa matokeo ya kazi za utafiti na ubunifu zinazofanywa na Taasisi zinainufaisha jamii na viwanda. Kwa kutambua mahitaji ya Umma kwa ujumla, Taasisi imeendelea kuboresha, sera mbalimbali za Taasisi zikiwemo sera za maktaba, maabara, Utafiti, na nyingine ambazo ziko katika hatua mbalimbali za uandaaji. Kwa sasa Taasisi inaandaa mkusanyiko wa watu wa viwanda na makampuni ili kujadili namna ya kushirikiana zaidi na kuona fursa za wanachuo kujishikiza (practical/field attachment) na kuboresha mitaala yetu kwa kutumia mawazo yao.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo;

Naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara mbalimbali zinazoendelea kufanikisha uendeshaji hatimaye kuwezesha maendeleo ya Taasisi. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipo washukuru; wewe mwenyewe, Mheshimiwa Mkuu wa Chuo na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya nne, Waziri Mkuu, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na mawaziri wengine kwa michango yao mikubwa wanayoonyesha katika kuiwezesha Taasisi yetu kuyafikia malengo yake. Tusingeweza kufikia hapa tulipo leo kama siyo kwa miongozo na misaada katika Taasisi yetu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo;

Ninapotathmini wahitimu hawa, siwezi kujizuia kujiuliza hivi ni nini historia ya kila mmoja katika mchakato wote wa elimu? Ni changamoto zipi, magumu yapi na nyakati gani za kukata tamaa ambazo kila mmoja ameweza kuzimudu hadi leo hii wanapohitimu masomo yao? Bila shaka, kila mmoja atakuwa na namna yake ya kujielezea kwa haya yote niliyouliza. Nawapongeza wote walioweza kuvumilia vikwazo vyote aidha kwa kukosa fedha, kuvutana katika kutetea kazi zao, kuahirisha masomo na mengine mengi hadi leo wanatunukiwa shahada zao; nawapongeza sana. Wakati mwingine, vitu vizuri na vya thamani vina historia ya kusema. Kwa kuangalia asili, tunaweza kujifunza mengi yanayoweza kutekelezeka katika maisha yetu. Na nina matumaini kwamba mtachukua vitu mlivyojifunza toka katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) ili kuvitumia katika kazi zenu, au kuanza upya kwa matarajio ya baadae.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo;

Wahitimu hawa ni wanasayansi, zaidi sana ni wanateknolojia na wabunifu. Ninachotaka wajifunze na elimu iwangie ni kutazama matone ya mvua. Katika kila tone la mvua kuna chembe chembe za udongo au vumbi. Mnatuambia kabla ya matone ya mvua kutengenezwa lazima chembe chembe za vumbi zikutane na zile za mvua na mnaziita "aerosols". Bila hizi chembe chembe za vumbi au udongo, mawingu ya mvua hayawezi kutengenezwa. Kila mmoja wetu si mkamilifu kwa namna moja au nyingine, na huu ndio ukweli wa maisha. Hakuna binadamu yeyote ambaye anajitosheleza kwa kila kitu; na kama umefanikiwa sana katika maisha, huwezi ukawa umefanikisha mwenyewe. Usikubali udhaifu wako ukurudishe nyuma. Tunakamilika tu pale ambapo tunafanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo;

Tunamshukuru Mungu kwa mahafali haya ya sita ambayo kama nilivyotamka mwanzoni jumla ya wahitimu **121** wa Shahada za Uzamili na Uzamivu watatunukiwa shahada zao. Ni matumaini yangu kuwa miaka yao waliyotumia kufanya kazi kwa bidii na kujitoa itakuwa imewafanya wa maana na mfano katika taaluma zao mara tu wakitoka leo nje ya lango la Taasisi hii. Tunawaombea matunda ya masomo yao yawafaidishe wenyewe, familia zao; na kutumika kutoa huduma katika jamii na viwandani na kuhakikisha kauli mbiu yetu ya "*Taaluma kwa jamii na viwanda*" na kwa msaada wa michango yenu hii nchi itakuwa ni ya ushindi hasa wakati huu ambao tunahamasisha ujenzi wa viwanda

kutoka uchumi wa kipato cha kati ngazi ya chini kwenda uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, Mabibi na Mabwana

Tanzania na hasa Arusha kipekee ni mwenyeji na kitovu cha kutoa elimu ya sayansi uhandisi, teknolojia na ubunifu. Kutokana na kuwepo katika eneo hili la Afrika katika mji wa Arusha na kupata kibali kama Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, tumejipanga vyema kutoa mapendekezo ya sera mbalimbali na Taasisi mbalimbali za Afrika kama vile Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na hata Umoja wa Afrika (AU) katika kuhamasisha masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ndani ya Afrika na nje ya mipaka ya Afrika. Mahusiano yetu na Taasisi/mashirika ya kimataifa yanafanya hili liwezekane kupitia miradi wa kujenga uwezo inayoendeshwa na Taasisi yetu chini ya usimamizi wa kikanda wa Afrika Mashariki. Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa msaada wao katika kutoa ufadhili kwa Wanafunzi **135** na leo wanahitimu **29** wa Uzamili na **6** wa Uzamivu. Kadhalika, vituo viwili vya umahiri chini ya Benki ya Dunia (WB) yaani WISE-FUTURES na CREATES kwa pamoja leo wana wanafunzi **30** wa Uzamili na **16** wa Uzamivu.

Pamoja na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Benki ya Dunia (WB) pia tunawashukuru wadau wengine kama German Academic Exchange Service (DAAD), Bodi ya mikopo Tanzania (HESLB), watu binafsi ambao wamewawezesha wahitimu hawa kufikia malengo yao.

Mheshimiwa Mkuu wa Chuo;

Kabla sijahitimisha hotuba hii, napenda kutoa pongezi kwa uongozi, kamati ya maandalizi ya mahafali ikiongozwa na Daktari Shubi Kaijage na wafanya kazi wote kwa maandalizi ya tukio hili muhimu. Kufanikisha tukio kama hili kunahitaji mipango thabiti na watu waliojitoa chini ya uongozi ulio makini. Kwa niaba ya baraza na mkusanyiko huu nawashukuru sana kwa kazi iliyotukuka ambayo sisi wenyewe ni mashahidi wa hilo na ninaamini kwamba wataendelea kufanya vizuri zaidi kwenye mahafali zitakazofuata. Mheshimiwa Mkuu wa Chuo, napenda kukushukuru tena kwa kujitoa na kutenga muda wako ili kufanikisha mahafali haya, na nawashukuru watu wote mlioungana nasi katika kuifanikisha shughuli hii muhimu.

Mungu ibariki Tanzania

Asanteni sana kwa kunisikiliza.